

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



“Nyamagana” Posta Road,  
S.L.P. 2599,  
MWANZA,  
Barua Pepe: rbcmwanza@pccb.go.tz.  
TANZANIA.

[www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

MWANZA – JULAI 06, 2020

## TAARIFA KWA UMMA

### RAIA WA CHINA MBARONI KWA RUSHWA

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mwanza, imemkamata raia wa china -SHENG BING LIN (40) kwa kosa la kushawishi na kutoa rushwa kiasi cha shilingi laki moja (100,000/=) ambapo ni kinyume na Kif cha 15 (1) (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Raia huyo wa China ambaye ni Msimamizi (Supervisor) wa Kampuni wa JX BETTING inayojishughulisha na michezo ya Bahati Nasibu kwa kutumia mashine maalum alishawishi na kutoa rushwa ya shilingi 100,000/= kwa Afisa Mtendaji wa Mtaa wa California - Nyegezi (jina limehifadhiwa) ili aweze kumrejeshea mashine yake ya kuchezeshea mchezo wa Bahati Nasibu.

Uchunguzi wa TAKUKURU Mkoa wa Mwanza ulibaini kwamba, Mchina huyo alishawishi na kutoa rushwa baada ya mashine yake moja ya kuchezeshea Bahati Nasibu (Betting) kukamatwa kwa makosa yafuatayo:

- Kutokuwa na kibali cha kuchezesha Bahati Nasibu,
- Kuchezesha Bahati Nasibu nje ya muda uliopangwa na Serikali **pamoja na**
- Kuwahusisha watoto chini ya umri wa miaka 18 katika mchezo huo.

Mashine hiyo ilikamatwa mwanzoni mwa mwezi Julai 2020 katika maeneo ya Nyegezi California na kupelekwa katika Kituo cha Polisi - Nyegezi. Hata hivyo, Mchina huyo alipokuwa akitakiwa kufika kituoni kutoa maelezo kuhusiana na kosa hilo hakuweza kutii amri hiyo na badala yake alipiga simu na kumshawishi Afisa Mtendaji apokee rushwa ili amrejeshee mashine yake.

Baada ya TAKUKURU Mkoa wa Mwanza kupokea taarifa hii ilifanya uchunguzi wa awali na kujiridhisha juu ya uwepo wa vitendo vya Rushwa. Baada ya hapo tuliandaa mtengo ambao ulifanyika, mnamo tarehe 2 Julai 2020 na Mchina huyo alikamatwa na Maafisa wa TAKUKURU katika maeneo ya La Cairo Hotel - Kirumba wakati anatoa rushwa ya shilingi laki moja kwa Afisa huyo wa Serikali.

SHENG BING LIN (40) anafanya kazi hii ya kucheza mchezo huo wa Bahati Nasibu (Betting) katika maeneo mbalimbali ya mjini na vijijini katika Mkoa Mwanza.

Uchunguzi wa tuhuma hii umekamilika na leo tarehe 06 Julai 2020 Mtuhumiwa atafikishwa Mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.

Aidha, tunampongeza mtumishi huyu mzalendo ambaye ametimiza wajibu wake wa kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa, kwa kutoa taarifa iliyofanikisha kukamatwa kwa mchina huyo. Tunaendelea kuwahimiza wananchi wote wa Mkoa wa Mwanza wasikae kimya wanapoona au hata kuhisi uwepo wa vitendo vya rushwa, bali wawe tayari kukemea vitendo vya rushwa pindi vinapojitokeza kwa kutoa taarifa TAKUKURU.

### **Kwa pamoja tutashinda vita dhidi ya rushwa**

**“Kwa taarifa za vitendo vya rushwa fika ofisi ya TAKUKURU iliyo karibu nawe, tumia TAKUKURU APP, piga simu ya dharura namba 113 au tuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au Piga \*113# fuata maelekezo” Huduma hii ni ya BURE.**

**IMETOLEWA NA:**

**SIGNED**

**DAUDI NDYAMUKAMA  
NAIBU MKUU WA TAKUKURU (M) MWANZA**